MAELEZO YA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. EDWARD N. LOWASSA (MB), KWA MHESHIMIWA RAIS WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA MIFUGO ULIOFANYIKA DODOMA, KWENYE UKUMBI WA MSEKWA - TAREHE 3 OKTOBA, 2006

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mhe. Dk. Shukuru Jumanne Kawambwa (Mb),

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. William Lukuvi (Mb),

Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, Mhe. Gideon Asimulike Cheyo (Mb),

Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb),

Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri,

Wakuu wa Mikoa na Wilaya,

Waheshimiwa Wabunge,

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Dodoma,

Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa,

Wahisani mbalimbali,

Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali,

Wafugaji,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

1. Napenda kuungana na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kukushukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali mwaliko wetu wa kuja kutufungulia mkutano huu wa wadau wa Sekta ya Mifugo. Mkutano huu ni mwendelezo wa mikutano ya wadau wa Sekta ya Mifugo nchini ili kuweza kujadili masuala muhimu ya namna ya kuboresha ufugaji.

Aidha, napenda kutumia nafasi hii kuushukuru uongozi wa mkoa na wananchi wa Dodoma kwa mapokezi yao mazuri kwako na kwa washiriki wa mkutano huu. Vilevile, nitumie fursa hii kuwashukuru wote mliokubali kuja kushiriki katika mkutano huu. Mahudhurio haya yanadhihirisha jinsi wadau wa sekta ya mifugo walivyodhamiria kuboresha sekta hii.

Mheshimiwa Rais,

2. Wakati nikiahirisha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Agosti 2006 hapa Dodoma, niliahidi kuitishwa kwa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo Mbeya tarehe 3/10/2006. Lakini kutokana na sababu mbalimbali imebidi mkutano huu ufanyike hapa Dodoma. Ahadi hii niliitoa baada ya mjadala uliokuwepo Bungeni kufuatia zoezi la Serikali la kuwahamisha wafugaji kutoka Pori la Akiba la Usangu hususan eneo la Ihefu kwenda maeneo mengine. Napenda kuipongeza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Rais,

3. Kutokana na uharibifu wa mazingira na uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji ambao ulianza kujitokeza mwishoni mwa mwaka jana hadi mwanzoni mwa mwaka huu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, alitoa Tamko la kudhibiti hali hiyo tarehe 1/4/2006. Katika kutekeleza Tamko hili, Serikali ilichukua hatua ya kuwahamisha wafugaji na mifugo yao kutoka katika maeneo ya hifadhi ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Tamko hili, niliunda Kamati Maalum ya Naibu Mawaziri watano ambao ni Mhe. Rita Mlaki (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) ambaye alikuwa Mwenyekiti, Mhe. Mathias Chikawe (Katiba na Sheria), Mhe. Dkt. Charles Mlingwa (Maendeleo ya Mifugo), Mhe. Celina Kombani (TAMISEMI) na Mhe. Mohamed Aboud (Usalama wa Raia). Napenda kutumia nafasi hii, kuipongeza Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo ilitoa mapendekezo ya muda mfupi na muda wa kati ya kushughulikia matatizo ya wafugaji nchini.

Mheshimiwa Rais,

4. Vilevile, niliwaagiza Mawaziri wa Wizara husika kukutana na kujadili mapendekezo ya ripoti hiyo. Napenda kukujulisha Mhe. Rais kuwa Waheshimiwa Mawaziri waliitisha kikao hicho kule Ngurdoto, Arusha tarehe 25 Agosti 2006 wakati wa Semina Elekezi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya na kikao kingine hapa Dodoma tarehe 8/9/2006.

Kikao hiki cha pili kiliwakutanisha pia Wakuu wa Mikoa minane na Makatibu Tawala wao kutoka mikoa ya Morogoro, Dodoma, Lindi, Mbeya, Iringa, Pwani, Rukwa na Ruvuma. Katika kikao hicho, kila Mkoa ulianisha maeneo ambayo wafugaji hao wangeweza kuhamia pamoja na gharama za kuweka miundombinu husika katika maeneo hayo. Hivyo, napenda kuwapongeza waheshimiwa Mawaziri kwa ripoti yao nzuri ambayo imeanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Rais,

5. Napenda pia kutumia nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa ya Lindi, Pwani na Mbeya na Wakuu wa Wilaya za Chunya, Kisarawe, Lindi Vijijini, Kilwa na Nachingwea walioweza kuainisha maeneo ya ufugaji ambayo tayari wafugaji wameanza kuhamia. Naamini Viongozi wa Mikoa na Wilaya nyingine nao wanaendelea kuainisha maeneo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Rais,

6. Nafurahi kutoa taarifa kwamba kati ya ng'ombe takriban 300,000 waliokadiriwa kuwepo katika bonde la Ihefu, zaidi ya ng'ombe wapatao 100,000 wamekwishahamishwa. Zoezi hili linaendelea kutekelezwa kwa uangalifu na umakini mkubwa kwa kuwashirikisha wafugaji wenyewe. Napenda kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kusimamia zoezi hili vizuri, zoezi ambalo walikabidhiwa na Wakuu wa Mikoa mingine. Naomba Mkoa uendelee na jitihada hizo hadi hapo zoezi litakapokamilika. Napenda pia kuwapongeza wafugaji kwa kukubali wito wa Serikali wa

kuwataka wahame kutoka Ihefu na nawaomba wale waliobakia huko nao wahame haraka bila bughudha yoyote.

Mheshimiwa Rais,

7. Nakushukuru sana tena kwa kukubali kwako kuja kutufungulia mkutano wetu huu. Kushiriki kwako ni changamoto kwetu sisi na wadau wote wa Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Rais, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa sasa nakukaribisha uongee na wadau wa Sekta ya Mifugo na kutufungulia mkutano wetu.

Karibu sana Mheshimiwa Rais